**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**MAWASILIANO**
***Mkuu wa shule***: *0753288498/0655273232*
***Makamu mkuu wa shule***: *0652846701*
***Mwalimu wa taaluma:*** *0657378754*
***E-mail***: *kiutasecondary@gmail.com*

Shule ya Sekondari Kiuta,
S. L. P 188,
NEWALA - MTWARA
…………….

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIUTA HALMASHAURI YA MJI NEWALA, MKOA WA MTWARA MWAKA……….**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao ,.................................................. amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule hii mwaka huu ………… katika Tahasusi ya ……………………….

Shule ya Sekondari **Kiuta** ipo umbali wa kilometa 12 kusini mashariki mwa mji wa Newala. Usafiri kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi Newala; nauli ni kati ya shilingi 3,000 kwa usafiri wa Noah/Hiece na bodaboda Tsh 8000 kutoka stendi kuu hadi shuleni.

Muhula wa masomo unaanza tarehe …………hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……….. ….mwisho wa kuripoti ni tarehe………..

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. MICHANGO.
   Michango yote inapaswa kulipwa kwenye akaunti ya shule Na: **70801200053** kwa jina la **Kiuta secondary school current account** katika benki ya NMB (**tafadhali hakikisha jina la Mwanafunzi limeandikwa kwenye pay slip**).

   Jedwali lifuatalo linaonyesha aina ya michango na kiasi:

| Na: | Aina ya Michango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Uendeshaji wa shule | 65,000. |
| 2. | Tahadhari | 5,000. |
| 3. | Nembo | 5,000. |
| 4. | Kitambulisho cha shule | 5,000. |
| **Jumla** | | **80,000.** |

   NB; Mwanafunzi **aje na Bank paying slip shuleni yenye jina lake inayoonesha malipo ya MICHANGO.**

2. SARE YA SHULE.
   Ifuatayo ni orodha ya sare ambazo mwanafunzi anapaswa kuwa nazo;

a) Sketi mbili ndefu za light blue (Esteem 1) urefu wa kufika hadi kwenye kifundo cha mguu (**aje nazo shuleni**).
b) Mashati mawili mawili (tetron) rangi nyeupe mikono mifupi **(aje nayo shuleni).**
c) Sweta la rangi ya dark blue moja au zaidi **(aje nayo shuleni).**
d) Gauni mbili za dark blue ndefu za kazi zenye urefu hadi kwenye kifundo cha mguu **aje nazo**. Mshono wa gauni ni solo, **mwanafunzi asishone dera halitapokelewa**.
e) Viatu vya ngozi nyeusi vya kamba jozi mbili –visigino vifupi **(aje navyo shuleni)**
f) Track rangi ya deark blue aje nayo isiyobana au kuonesha maungo ya ndani. **Rangi ya Track ni blue nyeusi ( dark blue) yenye ufito mweupe pembeni (aje nazo shuleni).**
g) Raba nyeupe jozi moja **(aje nazo shuleni).**
h) Soksi nyeupe jozi mbili na zaidi ndefu **(aje nazo shuleni).**
i) Kanga doti moja **(aje nayo shuleni).**
j) Taulo za kike za kutosha kulingana na mahitaji (**aje nazo shuleni**).
k) Tshirt za shule zinapatikana karibu na shule kwa gharama ya Tsh 15,000.
l) Shuka mbili za rangi ya pink **(aje nazo shuleni).**

## <u>MUHIMU</u>

**Mwanafunzi AJE na Bima ya Afya (CHF AU NHIF)** kama hana atapaswa hulipia sh, 50,400. kwa mwaka ili kupata Bima kutoka NHIF

3. VIFAA VYA KAZI.

a) Mchepuo wa HKL waje na;
  - ✦ Ruber Squezer/Mopper
  - ✦ Fagio gumu (Hard bloom)
  - ✦ Reki yenye mpini
  - ✦ Fagio laini(soft bloom)

b) Mchepuo wa HGK waje na;
  - ✦ Ruber Squezer/Mopper
  - ✦ Jembe lenye mpini
  - ✦ Brush za sink la choo

c) Mchepuo wa HGL waje na;
  - ✦ Jembe lenye mpini
  - ✦ Fagio laini (soft bloom)
  - ✦ Ruber Squezer/Mopper
  - ✦ Brush za sink la choo

d) Mchepuo wa HGLi waje na;
  - ✦ Ruber Squezer/Mopper
  - ✦ Fagio gumu (Hard bloom)
  - ✦ Jembe lenye mpini
  - ✦ Fagio laini (soft bloom)

e) Mchepuo wa HGFa waje na;
  - ✦ Ruber Squezer/Mopper
  - ✦ Fagio gumu (Hard bloom)
  - ✦ Jembe lenye mpini
  - ✦ Fagio laini (soft bloom)

Nb; Vifaa hivi vinapatikana maeneo ya karibu na shule

4. MAHITAJI KWA WANAFUNZI WA BWENI.

- Godoro, chandarua nyeupe au light blue na mto aje navyo.
- Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe.
- Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko aje nazo .
- Dawa ya chooni 5lt @ muhula aje nayo isiyozimuliwa wala kufunguliwa.
- Sanduku imara la bati (tranka la bati) aje nalo
- **Taa ya solar au Betri** kwa ajili ya kujisomea wakati umeme unapokosekana
- Taulo na kandambili

- Blanketi moja
- Fedha za kutosha kwa matumizi binafsi ya mwanafunzi ambayo ni muhimu kama vile; sabuni, mafuta, **pamba (pads za kutosha)** pamoja na fedha za kutumia awapo safarini ili asipate matatizo na vishawishi visivyo vya lazima.
- Nguo za ndani za kutosha
- Kwa wanafunzi wa kiislamu waje na juba la rangi nyeupe inayofunika mabega na mikono na baibui nyeusi pamoja na mtandio mweupe kwaajili ya msikitini.
- Ream **AINA YA DOUBLE A YA A4 MOJA KILA MUHULA**

5. VIFAA VYA DARASANI.

- Daftari kubwa (Counter Book Quire 3 & 4 zisizopungua 8 – 10 na daftari za kawaida kwa Summary zisizopungua 5 – 7 ( pia zinapatikana shule)
- Rula kubwa Cm 30 moja.
- Penseli na peni za kutosha.
- Mkebe wenye vifaa vyote.
- Kwa wanafunzi wa tahasusi za HGK na HGL waje na calculator ya kawaida.

**NB:** Vifaa hivi vinapatikana karibu na shule

Barua hii imeambatanishwa na sheria, kanuni na taratibu muhimu za shule. Taarifa binafsi ya mwanafunzi, fomu ya Hospitali na fomu ya mkataba ya kutoshiriki migomo. Fomu hizi ni lazima zijazwe na kurudishwa shuleni

6. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
c) Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku Preparation);
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
i) Kutunza mali za shule;
j) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;
k) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

7. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NIPAMOJA NA:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
vii. Uvutaji wa sigara;
viii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, au kuolewa;
ix. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
x. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xi. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiii. Kudharau Bendera ya Taifa;
xiv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xv. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xvi. Kufanya mawasilino nje ya utaratibu uliwekwa

8. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU.

a) Fomu ya uchunguzi wa afya (medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembeleamwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.
e) Cheti cha kuzaliwa(copy)
f) Cheti cha matokeo ya O-level(copy)
g) Leaving certificate(copy)

**MUHIMU:**

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum kutoka kwa Mkuu wa Shule. (kwa sababu ya Msiba au Ugonjwa pekee).

**NB:** ***kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. tafadhali upatapo ujumbe wowote kuhusu mwanafunzi/mtoto wako usitume chochote, ni vema ukawasiliana na uongozi wa shule kupata ukweli wa taarifa kupitia namba zilizopo kwenye fomu hii.***

**KWA NIABA YA WANAJUMUIYA YA SHULE YA SEKONDARI YA KIUTA NINAKUKARIBISHA SHULENI HAPA.**

**KARIBU SANA**

…………………………………….

**MKUU WA SHULE.**

**TAARIFA BINAFSI KUHUSU MWANAFUNZI.**

(***fomu hii ijazwe na mzazi / mlezi wa mwanafunzi na kuleta shuleni***)

1. Jina la mwanafunzi :
   ……………………………………………………………………….......
2. Kabila la mwanafunzi :
   …………………………………………………………….............
3. (a) Wilaya aliyozaliwa mwanafunzi :
   ………………………………………………………………………..
   (b) Mkoa
   ........................................................................................................
4. Dini ya mwanafunzi :
   ………………………………………………………………………..
5. Tatizo la mwanafunzi kiafya:
   ……………………………………………………………….................................
   ………………………………………………………………………………………
6. Tatizo la mwanafunzi kitabia:

…………………………………………………………………………………………

7. Jina kamili la Baba mzazi:

…………………………………………………………………………………………

Anuani kamili :

…………………………………………………………………………………………

Kazi yake : ……………………………………………………………......................

Umri: ………………………………………...........................................................

8. Jina kamili la mama mzazi :

…………………………………………………………………………………………..

Anuani kamili :

…………………………………………………………………………………………

Kazi yake: ……………………………………………………………..........................

Umri : .............................................................................................................................

9. Jina kamili la mtu/ mlezi anayemhudumia mwanafunzi kama vile kumlipia ada na vitu vingine

…………………………………………………………………………………………

10. Uhusiano wa mwanafunzi na mlezi

………………………………………………………………………………………....

Kazi yake: ……………………………………………………………........................

Umri: ...............................................................................................................................

11. Orodha ya ndugu watakao kuwa wanamtembelea mwanafunzi shule

| Na | Jina Kamili | Umri | Kazi | Anuani yake |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |

12. Baba na mama wa mwanafunzi wanaishi pamoja / wametengana **(kata isiyotakiwa).**

**AHADI:**

Mimi…………………………………………………………….............ambaye ni Mzazi/Mlezi mwanafunzi ………………………………………........
nimeyasoma na kuyaelewa maagizo ya kujiunga na shule hii na ninaahidi kulipa mishango yote na kumpa mahitaji mengine mwanangu aliyetajwa hapo juu mpaka anamaliza elimu ya sekondari

**KIUTA SEKONDARY SCHOOL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

TO:
The medical Officer,
……………………………………..
……………………………………..
………………………………………

FROM
THE HEADMISTRESS, KIUTA SECONDARY SCHOOL,
P. O BOX 188, NEWALA – MTWARA.
30/04/2025.
**Re: NAME** ……………………………………………………………………………

Please examine the above as to her/ his Physical and mental fitness for full time course of secondary Education at Kiuta Secondary School.

**MEDICAL CERTIFICATE.**

I have examine the above named students and consider that she / he is Physically and mentally fit/ unfit for a full time course of secondary Education at Kiuta Secondary school.

1. Eye sight: ……………………………………………………………….
2. Speech: ………………………………………………………………..
3. Hearing: ……………………………………………………………….
4. Venereal diseases: ……………………………………………………….
5. Neurosis: ………………………………………………………………
6. Pregnancy: ……………………………………………………………
7. Any other health problem: …………………………………………….

Doctor Remarks: ………………………………………………………….

Doctor's advice: …………………………………………………………..

Doctor's Name ………………………………………………………………………….

Signature ………………………………………..

Rubber stamp ……………………………………

**MKATABA WA KUTOSHIRIKI MIGOMO NA FUJO / VURUGU.**

(*Fomu hii ijazwe na kurudishwa shuleni).*

Mimi ……………………………………………………………ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha ………………………… Katika shule hii naahidi kutojihusisha kwa namna yoyote katika migomo, fujo au kosa lolote la jinai ambalo litahatarisha amani au litakalokuwa kinyume cha sheria, kanuni na taratibu za shule.

Endapo ilithibitika kuwa nimetenda kosa au makosa sitakuwa na pingamizi juu ya hatua za kinidhamu zitakazochukuliwa dhidi yangu kulingana na kanunu, taratibu na sheria za shule.

Jina la mwanafunzi …………………………………………………………

Sahihi ya mwanafunzi…………………………………………………………

Tarehe ………………………………………………………..........................

Jina la mzazi / mlezi……………………………………………………

Sahihi ya mzazi/ Mlezi ………………………………………………. ......

Tarehe ……………………………………………….............................

Anuani ………………………………………….........................................

Tarehe ………………………………………………………………………..

Mkuu wa shule,
Shule ya Sekondari Kiuta
S. l. P 188,
Newala – Mtwara**.**

**YAH: BARUA YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE.**

Ahsante kwa barua yako ya terehe ……………………………………….

(a) Nakubali / sikubali nafasi niliyopewa ya kidato cha tano kwa mwaka ……………………….
(b) Niko tayari/siko tayari kujiunga na shule ya Sekondari Kiuta.
(c) Niko tayari / siko tayari kufuata sheria, maagizo na masharti yote ya Kiuta sekondari.
(d) Nitahudhuria / sitahudhuria masomo yote ninayotakiwa kusoma hgapa shuleni.
(e) Nikishindwa kuhudhuria bila sababu ya msingi nifukuzwe shule.
(f) Nitaleta / sitaleta
   (i) Uthibitisho wa uraia / cheti cha kuzaliwa.
   (ii) Vitu vinavyohitajika kwa matumizi yangu
   (iii) Cheti cha afya.

……………………………………......... ..................................................................
JINA NA SAHIHI YA MWANAFUNZI JINA NA SAHIHI YA MZAZI / MLEZI